Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



# Mtu Huru Katika Karbala

Tukio lisilo na mwisho la Karbala huonyesha mfano mzuri wa mtu mmoja ambaye alijipa uhuru mwenyewe kutokana na pingu za uovu wa matamanio yake na baadae akaleta mfano halisi wa jina lake. Alikuwa akiitwa Hurr (mtu huru). Mwanzoni alikuwa miongoni mwa makamanda wa Yazid. Hata hivyo baada ya kutambua ubora wa ukweli, alitubia na kujiunga na safu ya Imamu al-Husain (a.s.). Akiwa amepigana kwa ushujaa sana katika safu ya Imamu (a.s.) dhidi ya Kuffar, alipata cheo cha juu sana cha Shahid. Katika dakika zake za mwisho, wakati Imamu al-Husain (a.s.) alipokuwa anavuja damu kutoka kwenye uso wake wenye nuru, alisema:

أَنْتَ حُرٌّ كَمَا سَمَّتْكَ أُمُّكَ, و أَنْتَ حُرٌّ فِي الدُّنْيَا وَ الآخِرَةِ

“Wewe ni Hurr (mtu huru) kama mama yako alivyo kuita; na uko huru katika ulimwengu huu na halikadhalika katika ulimwengu ujao.”

Mwanahistoria wa ki-Shi’a anayejulikana sana, Baqir Sharif al-Qarashi, katika kitabu chake, ‘*Hayat al-Imam al-Hussein* (*a.s.*)*’,* baada ya kunukuu maneno hayo hapo juu, alisema:

لَقَدْ كَانَ الْحُرُّ حُرًّا حِيْنَمَا تَغْلِبُ عَقْلُهُ هَوَاهُ

“Hakika Hurr alikuwa ‘mtu huru’ wakati akili yake iliposhinda juu ya muelekeo wake muovu (hawahu).”[1]

1. Baqir Sharif al-Qarashi, Hay□t al-Im□m al-Husein (a.s.), j. 3, uk.222.

**Source URL:** https://www.al-islam.org/fr/node/39637#comment-0